

**VIGEZO VYA KUWAPATA WASHIRIKI WA MAONESHO YA (21) YA NGUVU
KAZI/JUA KALI YA AFRIKA MASHARIKI YATAKAYOFANYIKA MKOANI MWANZA
TAREHE 09 - 19 DESEMBA, 2021**

Ili kupata wajasiriamali mahiri watakaoshiriki Maonesho ya Nguvu Kazi/ Jua Kali ya Afrika Mashariki Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi imeweka vigezo vifuatavyo vitakavyotumika kuchagua washiriki. Vigezo hivyo ni: -

1. Mshiriki mwenye kuzalisha bidhaa zenyenye ubora na kukidhi viwango vinavyokubalika kibashara na watakaotoa sura halisi ya bidhaa zinazotengenezwa Tanzania hususan katika Mkoa husika;
2. Mshiriki awe na vipeperushi na kadi ya utambulisho wa bidhaa (business cards) kama nyenzo muhimu ya kutangaza bidhaa na kutafuta masoko;
3. Mshiriki awe na bidhaa za ubunifu wa hali ya juu, kipaumbele ikiwa ni bidhaa zinazotokana na ngozi na mazao ya ngozi, nguo pamoja na bidhaa za kilimo zilizosindikwa, mifugo, Bahari, viungo (spices) na urembo;
4. Mshiriki awe na cheti cha uasili wa bidhaa (Certificate of origin) kinachotolewa na TCCIA na ZCCIA kwa upande wa Zanzibar;
5. Mshiriki awe na vifungashio vizuri vya bidhaa yake vinavyokubalika kimazingira;
6. Mshiriki awe tayari kujaza dodoso la taarifa za maendeleo ya biashara yake wakati wa Maonesho kama itakavyotakiwa na kurejesha dodoso kwa waratibu wa maonesho.

Mambo ya kuzingatia wakati wa kujaza fomu: -

1. Kila mjasiriamali anayekusudia kushiriki atatakiwa:
 - i. Kujaza fomu za ushiriki ambazo zinapatikana katika Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri/Manispaa Tanzania Bara;
 - ii. Kujaza fomu za tathmini ambazo zitapatikana wakati wa maonesho na zitajazwa kwa maelekezo yatakayotolewa
2. Mawasiliano kati ya wajasiriamali washiriki na Sekretariat ya Maonesho yafanyike kuitia viongozi wa Serikali na Vyama/Mitandao ya Wajasiriamali.